Kitabu cha Ayubu

MAZINGIRA
Miongoni mwa aina nyingi za vitabu vya Agano la Kale vipo vile vinavyojulikana kuwa vitabu vya hekima. Hivyo ni vitabu vya Ayubu, Mithali na Mhubiri, ingawa hata baadhi ya Zaburi na sehemu za vitabu vingine pia vinaweza kuhesabiwa kuwa ni maandiko ya hekima.

Maandiko ya hekima
Mungu alitumia aina mbalimbali za wahubiri na walimu ili kuwafundisha na kuwaongoza watu wake. Alitumia makuhani ili wafundishe na kuangalia sheria yake (Law 10:8-11; Kum 33:10; Mal 2:7), na manabii ili walete ujumbe wa kufunulia makusudi yake na kuwageuza watu waache dhambi zao na kumtii Mungu (Eze 2:3-5; Amo 3:1, 7-8; Mik 3:8). Pia alitumia walimu wa hekima. Watu hao ambao mara nyingine walijulikana kuwa *'wenye hekima'*, walikuwa miongoni mwa walimu maalumu katika Israeli (Yer 18:18; Isa 29:14). Hawakujidai kuwa wamepata mafunuo kuoka kwa Mungu, bali walieleza mambo ya maisha ya kila siku, na kama watu wenye imani, waliwafundisha wengine njia iliyo bora (Mhu 12:9-10).

Maandiko ya Biblia yanayotokana na walimu wa hekima yana aina mbili hasa. Wanaonyesha kwamba watu wenye hekima waliweza kutazama mambo ya maisha kwa njia mbalimbali. Mwalimu mmoja yule yule anaweza kutafakari mambo muhimu akiangalia sehemu tofauti. Kwa mfano, mwandishi wa Mithali anakubali kwamba kanuni za kawaida si lazimu zifae kwa kila jambo (Mit 26:4-5), ambapo waandishi wa Ayubu na Mhubiri wanatambua kwamba, ingawa kuna hali ya pekee au isiyo ya kawaida, kanuni za kawaida bado ni msingi wa mafundisho ya hekima (Ayu 28:20-28; Mhu 7:1-13).

Walimu wa hekima walikuwa wachaji wa Mungu waliotazama maisha pamoja na ugumu na furaha yote, ili wawasaidie watu wa Mungu watambue makusudi ya maisha waliyopewa na Mungu. Ingawa walitambua maisha ya baada ya kufa (Ayu 19:26), lengo lao kuu lilikuwa kushughulika na mambo yanayowakabili watu katika maisha yao ya sasa.

Kumfahamu Ayubu
Ayubu alikuwa tajiri aliyesoma na kumcha Mungu. Aliishi katika nchi ya Usi iliyokuwa mashariki ya Palestina. Alipopatwa na mfululizo wa maafa, marafiki zake walikazania kwamba shida zile lazima zilisababishwa na dhambi zake za siri. Ayubu alikataa maneno yao. Alijua kwamba hakuwa mtu mkamilifu, lakini pia alijua kwamba maoni ya kawaida ya desturi za nchi ile, kama yalivyoelezwa na marafiki zake, hayakueleza jambo lo lote. Majadiliano marefu yenye uchungu yaliyofuata yalijaza nafasi kubwa ya kitabu chote.

Elifazi (Ayubu 42:7) alikuwa ametoa mashtaka kwa Mungu kwamba watu humtumikia Mungu tu kwa sababu ya vitu wanavyoweza kupata kutoka kwake. Kama wangepata matatizo na shida wangemlaani (1:9-11; 2:4-5). Mungu akaruhusu maafa yaje juu ya Ayubu ili kupima uthabiti wa imani yake, na hivyo kuimarisha imani hiyo na kuongeza uzoefu wa Ayubu na Mungu (taz. Yak 5:11). Mateso ya Ayubu hayakuthibitisha hukumu ya Mungu juu yake, bali yalithibitisha matumaini yake katika Mungu na jinsi alivyomwamini.

Mkazo wa marafiki zake kwamba mateso au shida lazima vitokane na dhambi za mtu binafsi ulimfikisha Ayubu katika hali ambayo nusura ashindwe kuwavumilia zaidi. Lakini pia hali hiyo ilimsababisha amkaribie Mungu zaidi ambaye Ayubu alimwona kuwa tumaini lake la pekee. Alipomlalamikia Mungu, inawezekana kuwa alikosa alipotumia lugha isiyostahili, lakini kwa hali yo yote alipeleka malalamiko yake kwa Yule aliyehusika.

Mwisho aliridhishwa, si kwa sababu maswali yake yote yalijibiwa, bali kwa sababu alikutana na Mungu ambaye alimlilia. Inawezekana kwamba Ayubu hakuelewa makusudi ya Mungu, lakini alijifunza kwamba Mungu huyo ambaye hekima yake ilikuwa kubwa sana kuliko ufahamu wa wanadamu, alistahili kutegemewa. Mungu hakuhitaji kujitetea kwa wanadamu. Aliweza kufanya jambo lo lote alilopenda.

Mungu alipomthibitisha Ayubu, aliwaonyesha marafiki kwamba walikosa walipodai kwamba kila shida lazima ni matokeo ya dhambi za mtu binafsi. Pia alionyesha kwamba Elifazi alikosa alipodai kwamba watu wanamwabubu Mungu tu, kwa sababu anawapa mambo mema na fanaka. Ayubu alidumu kuwa mwaminifu kwa Mungu, ingawa alipoteza kila kitu, lakini mwisho Mungu alimbariki kwa mibaraka mikubwa kuliko alivyokuwa nayo hapo awali.

Maandishi ya Kitabu
Hakuna uhakika kuhusu wakati wa kuandikwa habari za Ayubu wala haijulikani mwandishi wa kitabu chake alikuwa nani. Lakini ukosefu wa mambo haya siyo kizuizi cha kuelewa ujumbe wa kitabu. Jambo muhimu ili kuelewa kitabu cha Ayubu siyo kumjua mwandishi wake au wakati wa kuandikwa kwake, bali jinsi kilivyoandikwa na muundo wake. Kitabu cha Ayubu ni kimojawapo cha maandiko ya Kiebrania yanyoitwa *'Maandiko ya Hekima'* na, ukitoa mwanzo na mwisho wake, ni maandiko ya mashairi.

Inafaa tukisoma kitabu cha Ayubu sawa sawa tunavyosoma vitabu vile vya Agano la Kale vyenye lugha ya mjazo wa masimulizi, maagizo ya haki au hotuba zenye wito. Hayo siyo kwa sababu kitabu kina alama za maandiko yenye hekima tulivyokwisha ona, bali kwa sababu kiliandikwa kwa mtindo wake. Haya yanaonekana katika kitabu chote, yaani katika masimulizi ya mwanzo wa kitabu, katika mifululizo ya majadiliano na katika mwisho wake wa kuvutia sana.

Kama ilivyo katika utunzi wo wote, msemo wake na aina ya utunzi wa maneno unastaajabisha wala maneno yake hayakukusudiwa kutafsiriwa moja kwa moja kila mara. Wala kitabu hiki hakikuandikwa ili kichunguzwe mstari kwa mstari, kwa sababu mara nyingine mstari mzima au hata mfululizo wa mistari kadhaa hutumiwa kueleza wazo moja tu la kimsingi. Mashairi ya Kiebrania kwa jumla na hasa maandiko ya hekima ya Kiebrania yalikuwa na maana ya pekee ambayo iliyafanya yatofautiane na maandiko mengine ya kawaida ya Agano la Kale. Kwa kuelewa maana hiyo zaidi, tazama pia maelezo yanayotangulia Zaburi na Mithali.

MUHTASARI

1:1-2:13	Elifazi amjaribu Ayubu
3:1-14:22	Mfululizo wa kwanza wa mahojiano
15:1-21:34	Mfululizo wa pili wa mahojiano
22:1-26:14	Mfululizo wa tatu wa mahojiano
27:1-31:40	Mfululizo wa Ayubu
32:1-37:24	Hoja za Elihu
38:1-42:17	Jibu la Mungu